


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO) LA MWAKA 2019

[SHERIA NDOGO]

Toleo hili la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo) la Mwaka 2019 ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Dodoma,  
....., 2020

ADELARDUS L. KILANGI,  
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 675 Limechapishwa Tarehe 13/9/2019

**SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA  
(SURA 407)**

**KANUNI**

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 60)*

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO), 2019

*Jina la Kanuni*

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

**SEHEMU YA PILI  
UTOAJI WA LESENI**

4. Katazo la kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha bila leseni.
5. Maombi na masharti ya leseni
6. Ushughulikiaji wa maombi.
7. Ukaguzi kabla ya kutoa leseni.
8. Leseni.
9. Kukataliwa kupewa leseni.
10. Ukataji rufaa.
11. Upandishaji daraja wa leseni ya SACCOS.
12. Ufutaji leseni.
13. Shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa.
14. Sehemu ya biashara.
15. Kufungua matawi.
16. Kuhamisha sehemu ya biashara.
17. Kuendesha huduma nje ya kituo.

SEHEMU YA TATU  
UTOSHELEVU WA MTAJI

18. Kiwango cha chini cha mtaji.
19. Katazo la kuhamisha mtaji.
20. Mgawanyo wa faida halisi.
21. Mfuko wa akiba.
22. Malipo ya gawio, riba na migao mingine.
23. Mpango wa kuongeza mtaji.

SEHEMU YA NNE  
UTAWALA

24. Muundo na majukumu ya Bodi.
25. Uhakiki na upotezaji sifa wa wajumbe wa Bodi.
26. Uteuzi na majukumu ya kamati ya mikopo.
27. Ajira na majukumu ya meneja wa SACCOS.

SEHEMU YA TANO  
SHUGHULI ZA UKOPESHAJI

28. Sera ya ukopeshaji
29. Maombi ya mkopo.
30. Idhini ya mkopo.
31. Mkataba wa mkopo.
32. Kuwasilisha sababu za kukataliwa maombi ya mkopo.
33. Dhamana ya mkopo.
34. Udhamini wa mkopo.
35. Miamala inayohusiana na watu wa karibu.
36. Upangaji wa kiwango cha riba, ada na adhabu.
37. Malipo ya mkopo kabla ya wakati.
38. Vigezo na masharti ya kushiriki mkopo.
39. Mikopo chechefu.
40. Uainishaji wa makundi na tengu la mikopo.
41. Limbikizo la riba ya mikopo chechefu.
42. Kurekebisha masharti ya mikopo.
43. Ufutaji wa mikopo.

SEHEMU YA SABA  
USIMAMIZI WA UKWASI, MALI NA DHIMA

44. Sera ya usimamizi wa mali na dhima.
45. Mpango wa dharura wa ukwasi.
46. Kiwango cha chini cha uwiano wa ukwasi wa mali.
47. Amana katika benki.
48. Ukopaji nje ya SACCOS.
49. Sera ya uwekezaji.
50. Masharti ya uwekezaji.

SEHEMU YA SABA  
HESABU NA UKAGUZI

51. Vitabu vya hesabu, kumbukumbu na mwaka wa fedha.
52. Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu.
53. Uwekaji wazi wa taarifa za fedha.
54. Uteuzi wa mkaguzi wa ndani.
55. Utoaji taarifa wa mkaguzi wa ndani.
56. Majukumu ya mkaguzi wa ndani.
57. Mpango wa ukaguzi wa ndani.
58. Kukodi mkaguzi wa ndani.
59. Ukaguzi wa nje.
60. Mkaguzi wa nje kuwafikia waajiriwa.
61. Kutoa taarifa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa.
62. Kuwasilisha taarifa ya ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.
63. Kubadilisha mkaguzi wa nje.
64. Kipindi cha mkaguzi wa nje.

SEHEMU YA NANE  
UKAGUZI NA USIMAMIZI

65. Ukaguzi wa SACCOS.
66. Uchunguzi.
67. Uwasilishaji wa taarifa.
68. Makubaliano ya pamoja ya usimamizi.
69. Utoaji wa amri ya zuio na katazo.
70. Usimamizi na kutwaa uendeshaji.
71. Ukomo wa usimamizi wa Benki au Mamlaka Kasimishwa.

SEHEMU YA TISA  
KUMLINDA MWANACHAMA

72. Masharti ya uwazi wa hisa, akiba na amana.
73. Uwazi kwa akaunti zenye riba.
74. Uwazi wa taarifa za ziada.
75. Uwazi wa mabadiliko ya masharti ya akaunti.
76. Uwazi katika utoaji wa mkopo.
77. Mfumo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro.
78. Uwazi kwa wadhamini wa mikopo.
79. Kukusanya au kufuatilia mkopo.
80. Elimu ya fedha.
81. Uzingatiaji wa sheria za kumlinda mlaji.

SEHEMU YA KUMI  
MASHARTI YA JUMLA

82. Mpango wa uendelezaji biashara.
83. Uwasilishaji wa taarifa za mikopo.
84. Ridhaa ya kubadilishana taarifa za mikopo.
85. Hatua za kiutawala.
86. Kuhama daraja kwa SACCOS
87. Kipindi cha mpito.
88. Makubaliano kati ya SACCOS na waajiri.

\_\_\_\_\_  
JEDWALI  
\_\_\_\_\_

TANGAZO LA SERIKALI Na. 675 Limechapishwa Tarehe 13/9/2019

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA,  
(Sura 407)

**KANUNI**

*(Zimetungwa chini ya kifungu 60 )*

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO), 2019

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

- Jina 1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo), 2019.
- Matumizi 2. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma ndogo za fedha wote walio katika Daraja la 3.
- Tafisiri 3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale muktadha unahitaji vinginevyo-
- Sura ya 407 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha;  
“wakala wa benki” maana yake ni biashara ya kutoa huduma za kibenki kwa wateja wa taasisi ya kibenki kwa niaba ya taasisi ya kibenki chini ya mkataba halali wa uwakala;
- Sura ya 197 “Benki” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;  
“tawi” maana yake ni sehemu ya biashara ya SACCOS tofauti na sehemu yake ya ofisi kuu, ambayo imeidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa kujiendesha kiutawala kama tawi;  
“amri ya zuio na katazo” “maana yake ni amri ya kiutawala

- inayochukuliwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa dhidi ya SACCOS ili kuzuia mambo yasiyo salama na yasiyo na tija yasitokee;
- Sura ya 185 “COASCO” maana yake ni Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika lililoanzishwa chini ya Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika;
- “Tume” maana yake ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika;
- “mtumiaji” maana yake ni mteja au mwanachama wa mtoa huduma ndogo za fedha ambaye anapata au anakusudia kupata huduma za mtoa huduma ndogo za fedha;
- “mtaji tete” maana yake ni hisa za wanachama zilizolipwa kwa ukamilifu, mfuko wa akiba za kisheria, limbikizo la ziada, misaada kwa ajili ya mtaji na michango ambayo haihamishiki na ambayo haikusudiwi kurejeshwa isipokuwa kama SACCOS imewekwa kwenye ufilisi;
- “taasisi ya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo” maana yake ni taasisi mahsusi inayokusanya na kuuza taarifa za mikopo za watu binafsi na taasisi;
- “Mamlaka Kasimishwa” maana yake itakuwa kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;
- “mikopo shirikishi” maana yake ni utaratibu ambao SACCOS moja au zaidi zinakopa kutoka taasisi za fedha kwa kudhamini SACOSS nyingine kulingana na makubaliano ya kimaandishi;
- Sura ya 394 “bima ndogo” maana yake itakuwa kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Bima;
- “karadha ndogo” maana yake ni shughuli za karadha ya fedha ambapo wastani wa thamani ya orodha ya mali inafikia shilingi milioni kumi na muda wa ukomo wa karadha hiyo hauzidi miezi ishirini na nne;
- “biashara ya huduma ndogo za fedha” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;
- “mkopo mdogo” maana yake ni mkopo uliotolewa kwa biashara ndogo, kaya na watu binafsi;
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya

- masuala ya fedha;
- Sura ya 423 “utakatishaji wa fedha” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Kupambana na Utakasishaji wa Fedha Haramu;
- “kituo cha huduma” maana yake ni sehemu ya biashara ya SACCOS zaidi ya tawi lililoidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa kuendesha shughuli chache za SACCOS;
- “sehemu ya biashara” maana yake ni tawi, ofisi, wakala, kituo cha huduma au huduma inayohama ya mtoa huduma ndogo za fedha iliyowazi kwa umma;
- “Rejesta” maana yake ni rejesta ya SACCOS zilizopewa leseni chini ya Sheria;
- Sura ya 211 “SACCOS” maana yake ni Chama cha ushirika wa akiba na mikopo kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika;
- “Daraja la 3” maana yake ni daraja la watoa huduma ndogo za fedha wanaojumuisha SACCOS.

SEHEMU YA PILI  
UTOAJI WA LESENI

- Katazo la kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha bila leseni
- 4.-(1) SACCOS haitafanya biashara yoyote ya huduma ndogo za fedha, bila SACCOS hiyo kupewa leseni na Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.
- (2) SACCOS yoyote itakayokiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa imetenda kosa, na ikitiwa na hatiani itapewa adhabu iliyoainishwa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria.
- Maombi na masharti ya leseni
- 5.-(1) SACCOS itaomba leseni ya kuendesha shughuli za huduma ndogo za fedha chini ya daraja A au B kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.
- (2) Maombi yaliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kwa ajili ya leseni daraja A yataambatishwa na-
- (a) nakala ya katiba ndogo ya SACCOS iliyothibitishwa kwa lengo la kuomba leseni;
- (b) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili



kilichotolewa na Tume;

- (c) majina kamili na anuani za wajumbe wa Bodi, wajumbe wa kamati ya usimamizi na maafisa wa SACCOS;
  - (d) wasifu binafsi na nakala zilizothibitishwa za vyeti vya taaluma na utaalum vya wajumbe wa Bodi na maafisa waandamizi;
  - (e) nakala ya sera ya ukopeshaji;
  - (f) nakala ya kitambulisho cha Taifa cha Tanzania, kitambulisho cha mpiga kura, hati ya kusafiria au kitambulisho chochote kinachokubalika na Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa kila mjumbe wa Bodi na maafisa wandamizi;
  - (g) picha ndogo mbili za “pasipoti” za wajumbe wa Bodi na maafisa waandamizi;
  - (h) ushahidi wa vifaa vya utunzaji na usalama wa fedha kwenye jengo la ofisi;
  - (i) azimio la mkutano mkuu la kuomba leseni;
  - (j) ushahidi kwamba SACCOS imeajiri au imeingia mkataba na mkaguzi wa ndani atakayewajibika, pamoja na majukumu mengine, katika ufuatiliaji pamoja na utekelezaji sahihi na madhubuti wa mfumo wa udhibiti wa ndani; na
  - (k) ushahidi kwamba SACCOS ina Mfumo wa Usimamaizi wa Taarifa.
- (3) Ombi lililorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kwa leseni za daraja B, litaambatishwa na-
- (a) vitu vyote vilivyoorodheshwa chini ya kanuni ndogo (2) ya Kanuni hizi;
  - (b) mpango wa biashara wa miaka mitatu ya uendeshaji unaojumuishwa:
    - (i) maelezo ya dhima;
    - (ii) muundo wa usimamizi;
    - (iii) bidhaa na huduma;
    - (iv) mipango ya kuongeza matawi pale inapohitajika;
    - (v) mkakati wa ukuaji; na
    - (vi) taarifa za makisio ya kiasi cha fedha kilichopo, taarifa za mapato, mtiririko wa fedha na makisio yaliyotumika katika

kufanya makadirio kwa miaka mitatu ya uendeshaji.

(c) sera za uwekezaji, rasilimali watu, akiba, ukwasi, fedha, ukusanyaji na taratibu za ndani na miongozo ya udhibiti; na

(d) ushahidi kwamba kuna kinga ya bima ya kutosha.

(4) Ombi la leseni litaambatishwa na malipo ya ada isiyorejeshwa ya ombi la leseni ya shilingi laki moja kwa leseni daraja A na shilingi laki tatu kwa leseni daraja B.

Ushughulikiaji wa maombi

6.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa itafanya maamuzi baada ya siku thelathini tokea siku iliyopokea maombi yaliyokamilika, na ikijiridhisha na maombi hayo, itatoa leseni.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imepokea nyaraka za maombi ya leseni ambazo hazijakamilika, kabla ya kushughulikia maombi hayo itamtaka mwombaji-

(a) kuwasilisha nyaraka au taarifa zinazokosekana au nyaraka za nyongeza; au

(b) kusahihisha au kurekebisha mapungufu yanayohusiana na masharti ya utoaji wa leseni.

Ukaguzi kabla ya kutoa leseni

7. Kabla ya kutoa leseni, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kufanya ukaguzi, vifaa vya mawasiliano, uhasibu na mifumo ya udhibiti wa ndani wa jengo la SACCOS.

Leseni

8.-(1) Endapo vigezo na masharti ya utoaji leseni yametimizwa, Benki au Mamlaka Kasimishwa itatoa leseni kwa SACCOS kwa namna inavyoanishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(2) Leseni iliyotolewa itaendelea kuwa halali isipokua kama itasitishwa au kufutwa kwa utaratibu ulioainishwa katika Sheria.

(3) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itafikia ukomo wake iwapo biashara haitaanza kufanyika ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kutolewa kwa leseni hiyo isipokuwa pale ambapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imeongeza muda huo kwa maandishi.

Kukataliwa kupewa leseni.

9.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kukataa kutoa leseni endapo-

- (a) mwombaji ameshindwa kukidhi vigezo na masharti yaliyoainishwa kwa ajili ya kupewa leseni; au
- (b) mwombaji ametoa taarifa za uongo au zinazopotosha.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imekataa kutoa leseni, itamjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za kukataa kutoa leseni ndani ya siku saba tokea tarehe ya uamuzi huo.

(3) Mleta maombi ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kuleta maombi upya iwapo amesahihisha mapungufu yaliyosababisha maombi ya awali kukataliwa.

Ukataji rufaa

10.-(1) Mwombaji ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya Benki au Mamlaka Kasimishwa chini ya kanuni ya 9 anaweza, ndani ya siku ishirini na moja tokea tarehe ya maamuzi hayo-

- (a) iwapo maamuzi yamefanywa na Mamlaka Kasimishwa, kukata rufaa kwenda kwa Benki; au
- (b) iwapo maamuzi yamefanywa na Benki, kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa kwa maandishi na itaeleza kwa uwazi-

- (a) aina ya rufaa;
- (b) sababu za rufaa; na
- (c) masuala mengine yoyote yanayohusika.

Tangazo la Serikali Na. 575 la 2019

(3) Waziri ataamua rufaa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri), 2019.

(4) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Benki itafanya maamuzi ya rufaa ndani ya siku sitini tokea tarehe ya kupokea rufaa hiyo.

(5) Katika kufanya maamuzi ya rufaa, Benki inaweza kumtaka mrufani kuwasilisha taarifa na nyaraka zote muhimu zinazounda msingi wa rufaa hiyo.

Upandishaji  
daraja wa  
leseni ya  
SACCOS

11.-(1) Endapo baada ya tathmini Benki au Mamlaka Kasimishwa imeridhika kwamba SACCOS yenye leseni daraja A inakidhi masharti ya awali ya mtaji wa SACCOS yenye leseni daraja B, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuelekeza SACCOS hiyo kuomba leseni chini ya daraja B.

(2) Endapo SACCOS itashindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1), bila sababu za msingi, Benki au Mamlaka Kasimishwa itachukua hatua kadiri inavyofaa ili kufanikisha utekelezaji huo.

Ufutaji leseni

12.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza, kwa kutoa noti kwa SACCOS, kufuta leseni endapo SACCOS-

- (a) imeacha kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha;
- (b) inakiuka masharti na vigezo vilivyoainishwa kwenye leseni;
- (c) imefungwa, imefilisiwa au imefutwa;
- (d) imefutiwa usajili kwa mujibu wa sheria husika ; au
- (e) imekiuka masharti ya Sheria.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa itatoa jina la mtoa huduma ndogo za fedha ambaye leseni yake imefutwa kwa ajili ya kuchapishwa katika *Gazeti* la Serikali na kwenye gazeti linalowafikia watu wengi ndani ya siku kumi na nne tokea kufutwa kwa leseni hiyo.

Shughuli  
zinazoruhusi  
wa na  
zisizoruhusiwa

13.-(1) SACCOS yenye leseni daraja A inaweza kufanya shughuli zifuatazo;

- (a) kutoa hisa za uanachama na za hiari;
- (b) kupokea akiba kutoka kwa wanachama wake;
- (c) kutoa mikopo kwa wanachama wake;
- (d) kufanya uwekezaji; na
- (e) shughuli nyingine kama itakavyoruhusiwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(2) SACCOS yenye leseni daraja B inaweza kufanya shughuli zozote kati ya zifuatazo:

- (a) shughuli zote chini ya kanuni ndogo ya (1) ya

kanuni hii;

- (b) kupokea amana kutoka kwa wanachama wake;
- (c) kutoa mikopo shirikishi;
- (d) kutoa karadha ndogo;
- (e) kutoa huduma za uwakala wa bima ndogo;
- (f) kuwa wakala wa benki baada ya idhini ya Benki au Mamlaka Kasimishwa;
- (g) kuwekeza katika mitaji;
- (h) kadi za kutolea fedha; na
- (i) shughuli nyingine kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Isipokua kama imeelekezwa vinginevyo na Benki au Mamlaka Kasimishwa, SACCOS yenye leseni haitafanya shughuli zifuatazo-

- (a) kuendesha akaunti ya biashara kwa wateja wake;
- (b) kupokea amana kutoka kwa watu wasio wanachama;
- (c) biashara ya kubadilisha fedha za kigeni;
- (d) uendeshaji wa biashara za nje ya nchi;
- (e) shughuli za udhamini;
- (f) kadi za mikopo;
- (g) maagizo ya malipo na uhamishaji wa fedha;
- (h) biashara nyingine isipokuwa kutoa huduma za kifedha kwa wanachama wake;
- (i) shughuli nyingine kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Sehemu ya biashara

14.-(1) Kila SACCOS itakuwa na-

- (a) sehemu ya au sehemu za biashara ikiwa na anuani sahihi kwa ajili ya kuendeshea biashara ya huduma ndogo za fedha; na
- (b) kuonesha kwa uwazi jina lake la biashara katika sehemu ya biashara.

Kufungua matawi

15.-(1) SACCOS yenye leseni daraja B inayokusudia kupanua huduma zake kwa kufungua tawi itaomba idhini kwa maandishi kutoka kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa.

- (2) Maombi yalioletwa chini ya kanuni ndogo ya (1)

yataambatishwa na yafuatayo-

- (a) eneo linalopendekezwa kwa ajili ya kufungua tawi;
- (b) lengo na madhumuni ya kufungua tawi jipya;
- (c) bajeti iliyochanganuliwa na chanzo cha fedha za uanzishaji wa tawi hilo;
- (d) makisio ya mizania na taarifa ya mapato na matumizi kwa muda wa miaka miwili baada ya tawi kuanza shughuli zake;
- (e) mapendekezo ya muundo wa tawi, majina na wasifu binafsi wa waajiriwa muhimu katika tawi; na
- (f) taarifa nyingine yoyote kama Benki au Mamlaka Kasimishwa itakavyohitaji.

(3) Katika kutathimini maombi chini ya kanuni ndogo ya (2), Benki au Mamlaka Kasimishwa itazingatia-

- (a) uwezo wa kujiendesha wa tawi linalopendekezwa;
- (b) uwezo wa kifedha wa SACCOS kuendesha tawi linalopendekezwa;
- (c) endapo SACCOS inakidhi kiwango cha chini cha mtaji unaohitajika;
- (d) uweledi na uwezo wa watendaji wa tawi linalopendekezwa;
- (e) endapo tawi linalopendekezwa linakidhi vigezo vya usalama angalau kwa kiwango cha chini; na
- (f) kigezo kingine chochote kadiri itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(4) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kufanya ukaguzi wa jengo la tawi linalopendekezwa kabla ya kuanza uendeshaji.

(5) SACCOS yenye leseni daraja A haitaruhusiwa kufungua tawi.

Kuhamisha  
sehemu ya  
biashara

16.-(1) SACCOS ambayo inadhamiria kuhamisha sehemu ya biashara yake, itaomba idhini kwa maandishi kutoka kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa na maombi hayo yataambatishwa na taarifa zifuatazo:

- (a) sababu za kuhamisha biashara;
- (b) mpango kwa ajili ya kulipa au kuhamisha madai, mali na madeni;

- (c) ukamilishaji wa maandalizi ya sehemu mpya ya biashara; na
  - (d) taarifa nyingine yoyote kama Benki au Mamlaka Kasimishwa itakavyo elekeza.
- (2) SACCOS itakayoshindwa kuzingatia masharti ya kanuni hii itakuwa imetenda kosa.

Kuendesha huduma nje ya kituo

17.-(1) SACCOS haitafungua au kutoa huduma nje ya kituo bila idhini ya maandishi ya Benki au Mamlaka Kasimishwa iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(2) Ombi la idhini lililotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) litaambatanishwa na yafuatayo-

- (a) taarifa ya hali ya usalama na nafasi iliyopo kwa ajili ya SACCOS kutoa huduma; na
- (b) taarifa nyingine zozote kama Benki au Mamlaka Kasimishwa inavyoweza kuhitaji.

#### SEHEMU YA TATU UTOSHELEVU WA MTAJI

Kiwango cha chini cha mtaji

18.-(1) SACCOS yenye leseni daraja A itanza kufanya biashara na kuhakikisha muda wote ina mtaji tete usiopungua shilingi milioni kumi.

(2) SACCOS yenye leseni daraja B itanza kufanya biashara kwa kuhakikisha muda wote ina mtaji tete usiopungua shilingi milioni mia mbili.

- (3) Kila SACCOS itatakiwa muda wote kuwa na-
- (a) mtaji tete usiopungua asilimia nane ya jumla ya mali zote;
  - (b) mtaji taasisi usiopungua asilimia sita ya jumla ya mali zote; na
  - (c) mtaji taasisi halisi usiopungua asilimia sita ya jumla ya mali zote.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo za (1) na (2), Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuhitaji kiwango cha juu zaidi ya kima cha chini cha mtaji au viwianishi vya utoshelevu vya mtaji kwa SACCOS iwapo SACCOS-

- (a) inaweza kupata hasara kutokana na upungufu wa mtaji;

- (b) ina mazingira hatarishi ya hali ya juu;
- (c) inakuwa na kiwango cha juu au kiasi kikubwa cha mali zenye ubora duni; au
- (d) inakuwa kwa haraka bila kuwa na kiwango cha kutosha cha mtaji na udhibiti wa vihatarishi.

Katazo la kuhamisha mtaji

19. Isipokuwa kama imeidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa, SACCOS haitahamisha fedha kutoka kwenye mtaji tete au mfuko wa matengo ya kisheria endapo uwiano wa mtaji taasisi ni pungufu ya uwiano wa chini unaohitajika.

Mgawanyo wa faida

20. Kwa mujibu wa kanuni zake, SACCOS inaweza kugawa kiasi chochote kilichosalia cha mapato halisi baada ya gharama zote kulipwa na masharti ya mtaji yamefikiwa kwa ajili ya malengo yafuatayo-

Sura ya 211

- (a) gawio la hisa kwa njia ya fedha taslimu au kuweka katika hisa za wanachama;
- (b) mchango kwa ajili ya mfuko wa maendeleo au akaunti ya mtaji wa mpito ;
- (c) mchango kwa ajili ya hisani, elimu, matibabu au malengo mengine kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.
- (d) kulipa tunzo kwa wajumbe wa Bodi na maafisa wengine wasiolipwa mishahara; na
- (e) malipo mengine kama yatakavyoidhinishwa na mkutano mkuu wa mwaka .

Mfuko wa akiba

21. Kila SACCOS itakuwa na mfuko wa akiba na mtaji taasisi kwa kutenga angalau asilimia ishirini ya mapato halisi baada ya matumizi na gharama zote kulipwa.

Malipo ya gawio, riba na migao mingine

22.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria, kila SACCOS itaweka katika kanuni zake malipo ya lazima ya gawio, riba au aina nyingine ya mgao kwa wanachama wake ikijumuisha namna na kipindi ambacho malipo hayo yatalipwa.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), hakuna malipo ya gawio au mgawo wa namna nyingine yoyote utakaolipwa



kutokana na ziada halisi, isipokuwa-

- (a) mtaji taasisi na mtaji taasisi halisi ikilinganishwa na uwiano wa jumla ya mali unafikia sharti la kiwango cha chini kilichowekwa;
- (b) kiasi cha akiba ya kisheria kinatosha kufidia limbikizo la hasara la SACCOS;
- (c) kiasi cha akiba ya kisheria, tengo la mikopo isiyolipika na mfuko wa kukombolea hisa vimetengwa; na
- (d) baada ya kupata ridhaa ya mkutano mkuu na ridhaa ya Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Mpango wa kuongeza mtaji

23.-(1) Endapo SACCOS imeshindwa kufikia masharti ya kiwango cha chini cha mtaji kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi, SACCOS hiyo itatakiwa ndani ya siku sitini za mapungufu hayo, kuwasilisha Benki au Mamlaka Kasimishwa mpango wa kuongeza mtaji wake.

(2) Mpango wa kuongeza mtaji ulioainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), kwa uchache, utaeleza yafuatayo-

- (a) hatua zitakazochukuliwa na uongozi ili mtaji kurudi katika kiwango cha chini kinachohitajika;
- (b) muda unaohitajika ili mtaji kurudi katika kiwango cha chini kinachohitajika;
- (c) kiwango cha mtaji kinacholengwa kufikiwa kila mwishoni mwa robo mwaka; na
- (d) taarifa nyingine yoyote kama Benki au Mamlaka Kasimishwa itakavyohitaji.

(3) Endapo SACCOS imeshindwa kufikia kiwango cha chini cha mtaji na imeshindwa kuwasilisha au kutekeleza mpango wa kuongeza mtaji, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuchukua hatua za kiusimamizi kama itakavyoona inafaa.

#### SEHEMU YA NNE UTAWALA

Muundo na majukumu ya Bodi

24.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria, uongozi wa SACCOS utakuwa kama inavyoelezwa katika Sheria ya Vyama Vya Ushirika, Kanuni zake na kanuni za SACCOS.

Sura ya 211

Sura ya 211

(2) Kila SACCOS itakuwa na Bodi itakayoundwa na angalau wajumbe watano watakoachaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2), Bodi ya SACCOS yenye leseni ya daraja B itakuwa na angalau wajumbe wawili wenye ufahamu wa masuala ya fedha, usimamizi wa biashara, uhasibu, huduma ndogo za fedha au uchumi.

(4) Pamoja na wajibu ulioelezwa chini ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika, Bodi iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (2)-

- (a) itahakikisha SACCOS inafanya shughuli zake kwa ufanisi na inazingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi na sheria nyingine yoyote husika;
- (b) itatunga sera sahihi kwa ajili ya mikopo, usimamizi wa ukwasi na mali, rasilimali watu, uwekezaji, akiba, fedha, utunzaji taarifa, na sera nyingine kama itakavyoamuliwa na Bodi;
- (c) itatoa mapendekezo kwa ajili ya SACCOS kukopa;
- (d) itahakikisha hesabu za SACCOS zinaandaliwa na kukaguliwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni hizi na masharti;
- (e) itaweka viwango vya riba kwa ajili ya mikopo, akiba na amana;
- (f) itapendekeza malipo ya gawio la hisa katika mkutano mkuu wa mwaka, kwa idhini ya Benki au Mamlaka Kasimishwa;
- (g) baada ya kukasimishwa na mkutano mkuu wa mwaka, kuteua kamati ya mikopo, na kamati nyingine yoyote husika miongoni mwa wajumbe wa Bodi au wanachama wenye sifa;
- (h) kwa msaada wa menejimenti, itaandaa, mpango

wa kurithisha madaraka na uokozi wa majanga na kuhakikisha mipango hiyo inajaribiwa mara kwa mara;

- (i) itatoa mwongozo wa usimamizi na mwelekeo wa sera ya SACCOS;
- (j) itahakikisha SACCOS inaweka tengo la kutosha kwa ajili ya mikopo isiyolipika inavyoelekezwa na Kanuni hizi;
- (k) itapitia bajeti ya mwaka ya SACOSS na kutoa mapendekezo kwa mkutano mkuu kwa ajili ya kupata idhini;
- (l) inathibitisha idhini ya mikopo yote iliyoombwa na wajumbe wa Bodi na wajumbe wa kamati, menejimenti ya SACCOS na watu wenye mahusiano nao;
- (m) itahakikisha uwekezaji wa ukwasi wa ziada unakidhi matakwa ya Sheria, Kanuni hizi na unafanywa kwa kuzingatia sera ya uwekezaji ya SACCOS;
- (n) itahakikisha SACCOS inafanya shughuli zake kwa ufanisi na inazingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi na sheria nyingine yoyote husika;
- (o) itaajiri meneja na kuwandalia mikataba ya kazi; na
- (p) itasimamia ufunguaji na matumizi ya akaunti za benki za SACCOS.

Uhakiki na upotezeshaji sifa wa wajumbe wa bodi

25.-(1) SACCOS haitafanya biashara isipokuwa pale ambapo wajumbe wake wa Bodi wamefanyiwa uhakiki na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Sura ya 211

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kumwondolea sifa mjumbe wa bodi ya SACCOS pale ambapo itabaini kwamba mjumbe huyo-

- (a) hana sifa zinazotakiwa na Sheria na Kanuni hizi;
- (b) amejihusisha au anahisiwa kukosa uaminifu au kuwa mdanganyifu katika shughuli zake;
- (c) ana mikopo chechefu au madeni mengine ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya siku tisini;
- (d) ana mgongano wa maslahi ambao utaathiri uwezo wake wa kufanya kazi kama mjumbe wa Bodi; na
- (e) amevunja masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imemwondolea sifa mjumbe wa Bodi, mjumbe huyo ataacha kufanya shughuli yoyote ya Bodi akisubiri taratibu za kufutiwa mjumbe kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika na Kanuni zake.

Uteuzi na majukumu ya kamati ya mikopo Tangazo la Serikali Na. 115 la 2016

26.-(1) Kila SACCOS itateua Kamati ya Mikopo kwa lengo la kuwezesha uendeshaji wa shughuli zake kuendana na Kanuni za Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo na Kanuni za SACCOS.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), kamati ya Mikopo itakuwa na majukumu yafuatayo-

- (a) kupitia maombi ya mikopo na kufanya maamuzi kwa kuzingatia sera ya mikopo;
- (b) kuhakikisha dhamana ya kutosha inatolewa kwa kila mkopo na SACCOS ina haki au mamlaka juu ya dhamana hiyo mpaka mkopo wote utakapolipwa;
- (c) kufuatilia marejesho ya mikopo;
- (d) kuhakikisha mikopo inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa;
- (e) kufanyia kazi maombi ya wanachama kuhusu marekebisho ya vigezo na masharti ya mkopo endapo mabadiliko hayo yanaendana na sera ya mikopo ya SACCOS;
- (f) kutoa ushauri kwa wanachama kuhusu matumizi

- sahihi ya mikopo;
- (g) kupitia sera ya mikopo angalau mara moja kwa mwaka;
- (h) kutoa majibu ya hoja za wakaguzi wa nje na wa ndani, kamati ya usimamizi na Benki au Mamlaka Kasimishwa; na
- (i) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa kuzingatia Sheria na Kanuni hizi.

Ajira na  
majukumu ya  
Meneja wa  
SACCOS

27.-(1) Kila SACCOS itaendeshwa na watu walio na sifa na weledi kuendana na masharti ya Kanuni za Ushirika (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo) na sera yake ya rasilimali watu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu alieajiriwa kushika nafasi ya meneja, pamoja na majukumu aliyonayo chini ya Kanuni za Jumla za SACCOS atakuwa na majukumu yafuatayo-

- (a) kuhakikisha mifumo ya uendeshaji na utoaji wa taarifa ina ufanisi, ina uhakika na inarahisisha mawasiliano;
- (b) kuandaa bajeti ya mwaka na mpango mkakati wa biashara kwa kushauriana na wajumbe wa Bodi;
- (c) kusimamia masuala yote ya watumishi ikiwemo maendeleo ya rasilimali watu na mafunzo;
- (d) kuhifadhi na kuandaa taarifa sahihi za fedha kwa wakati;
- (e) kuwasilisha taarifa za uendeshaji katika mikutano ya bodi;
- (f) kuruhusu matumizi kulingana na bajeti iliyopitishwa na Bodi;
- (g) kuisaidia Bodi kupanga viwango vya riba, ada na gharama za bidhaa na huduma zote zinazotolewa;
- (h) kuhakikisha kuna ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo, utoaji wa akiba na gharama za uendeshaji;
- (i) kusimamia ufunguaji na matumizi ya akaunti za benki;
- (j) kuandaa na kuwasilisha taarifa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa wakati;
- (k) kutekeleza mapendekezo yaliyomo katika taarifa

za ukaguzi wa nje, ukaguzi wa ndani na taarifa za usimamizi;

(l) kuhakikisha matakwa ya Sheria, kanuni, sera, taratibu, masharti na taratibu za maadili zinazingatiwa; na

(m) kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Bodi.

(3) Licha ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), mtu aliyeajiriwa kushika nafasi ya meneja wa SACCOS-

(a) ikiwa ni SACCOS yenye leseni ya daraja A, atakuwa na angalau cheti cha elimu ya sekondari; na

(b) ikiwa ni SACCOS yenye leseni ya daraja B, atakuwa na angalau stahhada ya fedha, uhasibu, utawala au fani nyingine zinayohusiana na hizo.

(4) Kila SACCOS itahakikisha kuwa hakuna mtu anayeteuliwa kuwa meneja wa SACCOS isipokuwa pale ambapo mtu huyo amefanyiwa uhakiki na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

#### SEHEMU YA TANO SHUGHULI ZA UKOPESHAJI

Sera ya ukopeshaji

28.-(1) Kila SACCOS itakuwa na sera ya ukopeshaji inayoendana na Sheria na Kanuni hizi.

(2) Sera inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1), kwa uchache itajumuisha yafuatayo:

(a) taratibu za ukopeshaji na nyaraka zinazohusika;

(b) masharti ya kukidhi kupata mkopo;

(c) aina za mikopo na dhamana zinazokubalika;

(d) ukomo wa mikopo ikijumuisha kiwango cha juu cha mkopo kwa mkopaji;

(e) vigezo na masharti ya mkopo kama viwango vya riba, ada, tozo na idadi ya marejesho;

(f) adhabu au ada kwa marejesho yaliyocheleweshwa;

(g) ukomo wa mkopo ukilinganishwa na thamani ya dhamana;

(h) tathimini ya uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo;

- (i) vigezo na masharti vya mikopo kwa maafisa na waajiriwa;
- (j) ukomo wa juu wa uidhinishaji mikopo kwa kamati ya kitaalamu na kamati ya mikopo;
- (k) masharti ya udhamini wa mkopo;
- (l) ufuatiliaji na tathimini ya ubora wa mikopo;
- (m) kipindi kinachotolewa kabla ya kuanza kurejesha mkopo, kama kipo;
- (n) utaratibu wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa mikopo.
- (o) vigezo na taratibu za kurekebisha masharti ya mikopo na uhamishaji wa hisa za hiari za mwanachama ikijumuisha idhini na ruhusa;
- (p) kigezo na taratibu za kuidhinisha na kuruhusu kufuta mikopo isiyolipika;
- (q) muda wa kulipa mkopo ikizingatiwa kwamba muda huo hautazidi miaka mitano;
- (r) fomu husika zinazotumika kwa ajili ya maombi ya mkopo; na
- (s) taarifa nyingine yoyote muhimu.

Maombi ya  
mkopo

29.-(1) SACCOS itahakikisha kwamba kila mwanachama anayekusudia kupata mkopo anawasilisha maombi kwa kutumia fomu maalum iliyoandaliwa na SACCOS.

(2) Fomu inayorejewa na kanuni ndogo ya (1) kwa uchache itajumuisha yafuatayo-

- (a) jina kamili la mwombaji;
- (b) tarehe ya kuzaliwa au tarehe ya usajili;
- (c) sehemu ya makazi au sehemu ya biashara;
- (d) kazi au aina ya biashara;
- (e) dhumuni la mkopo;
- (f) sekta ya kiuchumi;
- (g) kiasi cha mkopo kinachoombwa;
- (h) dhamana inayotolewa;
- (i) hali ya ndoa;
- (j) idadi ya wategemezi;
- (k) sehemu ya ajira;
- (l) kipato cha sasa;
- (m) matumizi na mali;
- (n) mikopo mingine inayodaiwa; na

(o) taarifa nyingine zinazoweza kuhitajika.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo (2), fomu ya maombi ya mkopo itajumuisha sharti kwamba mleta maombi atatoa ridhaa na tamko kwamba taarifa zake za mikopo zinaweza kutolewa kulingana na masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

Idhini ya  
mkopo

30.-(1) SACCOS haitatoa mkopo bila idhini ya kamati ya mikopo.

(2) Kamati ya mikopo haitaidhinisha mkopo isipokuwa kama mkopo wote au sehemu kubwa ya mkopo huo umedhaminiwa.

Mkataba wa  
mkopo

31.-(1) SACCOS itafanya tathmini maombi ya mkopo kwa kuzingatia sera yake ya ukopeshaji na endapo itaridhika kwamba mkopaji anakidhi masharti ya mkopo na ana uwezo wa kurejesha mkopo, itaingia mkataba wa mkopo na mkopaji.

(2) Mkataba wa mkopo unaorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kwa uchache itajumuisha yafuatayo;

- (a) kiasi cha mkopo;
- (b) kiwango cha riba cha kawaida au kilichotajwa kwa mwaka;
- (c) ada zote nyingine zitakazotozwa;
- (d) kiwango halisi cha riba cha mwaka kinachojumuisha ada zote zitakazotozwa;
- (e) ratiba ya marejesho ya mkopo inayojumuisha idadi ya marejesho, kiasi cha kila rejesho kikiainisha tofauti mkopo, riba, ada na tarehe ya rejesho;
- (f) jumla ya malipo mpaka mkopo wote utakapokuwa umelipwa;
- (g) njia ya kukokotoa kiwango cha riba;
- (h) adhabu ya ucheleweshaji malipo;
- (i) ada za ufuatiliaji mkopo, tozo au gharama;
- (j) notisi inayoonesha maslahi katika dhamana iliyotumika kudhamini mkopo;
- (k) saini za mkopaji na mtoa huduma ndogo za fedha;
- (l) kiasi cha akiba au hisa kinachohitajika na iwapo fedha zilizopatikana zinaweza kutumika kulipa



- marejesho ya mkopo uliocheleweshwa; na  
(m) masuala mengine yoyote husika yatakayowekwa wazi kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Kuwasilisha sababu za kukataa maombi ya mkopo

32. Endapo maombi ya mkopo yamekataliwa, SACCOS itampatia mleta maombi ya mkopo sababu za kukataa maombi hayo ndani ya siku saba.

Dhamana ya mkopo

33.-(1) Mwanachama anaweza kudhamini mkopo kwa kutumia hisa za hiari, akiba, amana ya muda maalum au mali, ikiwa mkopo huo hautazidi asilimia kumi ya mtaji tete.

(2) Endapo mkopo haujadhaminiwa kikamilifu na hisa za hiari, akiba, amana za muda au mali, mkopo huo hautazidi asilimia tano ya mtaji tete.

(3) kabla ya kutoa mkopo, SACCOS itahakikisha kwamba-

- (a) nyaraka za dhamana ya mkopo ni sahihi au zimesajiliwa;
- (b) endapo mmiliki wa dhamana sio mkopaji, mkopaji atapaswa kuwa na kibali cha kimaandishi kinachomruhusu kutumia dhamana hiyo kudhamini mkopo;
- (c) inatunza rejesta ya dhamana zote ambayo inajumuisha taarifa zote muhimu za dhamana; na
- (d) hisa za uanachama hazitatumiki kama dhamana kwa mkopo unaotolewa na SACCOS.

Udhamini wa mkopo

34.-(1) Mwanachama anaweza kudhamini mkopo unaotolewa kwa mwanachama mwingine ikiwa mwanachama huyo ana dhamana za kutosha ikiwemo hisa za hiari, akiba, amana na dhamana nyingine zinazokubalika.

(2) SACCOS itamfahamisha vya kutosha kila mdhamini kuhusu wajibu wake kabla ya kusaini makubaliano ambayo yatamfanya aweze kuwajibika kama mdhamini.

(3) Endapo SACCOS itakusanya malipo ya mkopo kutoka kwa mdhamini, SACCOS itatoa hati ya maandishi kukiri kupokea marejesho ya mkopo.

Miamala  
inayohusiana  
na watu wa  
karibu

35.-(1) SACCOS haitatoa mkopo kwa mjumbe wa bodi au kamati au watu wa karibu wa mjumbe wa bodi au kamati isipokuwa kama mkopo huo umeidhinishwa na wajumbe wengi wa bodi.

(2) Mjumbe wa bodi au kamati hatahudhuria kikao wakati mkopo wake ukiwa unajadiliwa na wajumbe.

(3) SACCOS haitatoa mkopo kwa mwajiriwa au ndugu wa mwajiriwa isipokuwa kama mkopo huo umeidhinishwa na kamati ya mikopo.

(4) SACCOS haitatoa mkopo kwa afisa, mwajiriwa au ndugu wa afisa au mwajiriwa kwa vigezo na masharti ambayo ni mepesi zaidi kwa kulinganisha na yale yanayotolewa kwa wanachama wengine.

(5) Kiwango cha jumla cha mkopo kwa waajiriwa na maafisa hakitazidi asilimia tano ya mali zote za SACCOS.

(6) Hakuna afisa au mtu mwenye uhusiano wa karibu naye atapokea kitu chochote cha thamani au fidia inayohusiana na mkopo uliotolewa na SACCOS bila idhini ya mkutano mkuu na idhini ya Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Upangaji wa  
kiwango cha  
riba, ada na  
adhabu

36. Isipokuwa pale ambapo mkutano mkuu umeelekeza vinginevyo, Bodi inaweza kupanga viwango vya riba, ada na adhabu kwa mkopo ambavyo vitakuwa vikifanyiwa mapitio mara kwa mara.

Malipo ya  
mkopo kabla  
ya wakati

37.-(1) Mwanachama anaweza kulipa mkopo wote au sehemu ya mkopo siku yoyote ya kazi kabla ya muda wa kulipa mkopo kufika, bila kuadhibiwa.

(2) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), endapo mkopo umelipwa wote kabla ya muda wa kulipa mkopo kufika, mkopaji hatatakiwa kulipa riba kwa kipindi kilichobakia baada ya mkopo kulipwa.

Vigezo na  
masharti ya  
kushiriki  
mikopo

38.-(1) SACCOS yenye leseni daraja B inaweza kukopa au kukopesha SACCOS nyingine kwa dhumuni la kukidhi upungufu wa ukwasi kwa kuzingatia kwamba-

(a) SACCOS inayokopa haitazidi ukomo wa kukopa nje kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi;

(b) wajumbe wa bodi ya SACCOS wameidhinisha

- ukopaji au ukopeshaji kwa SACCOS nyingine;
- (c) vigezo na masharti ya kukopa au kukopesha vitathibitishwa na makubaliano ya maandishi yaliyosainiwa baina au kati ya SACCOS zinazoshiriki na makubaliano hayo yataidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa; na
- (d) masharti ya kanuni ya 33 na 34 yatazingatiwa kama yalivyo pamoja na marekebisho madogo yanayoweza kufanyika.

(2) Endapo SACCOS siyo mkopeshaji halisi, SACCOS hiyo itatakiwa-

- (a) kushiriki kwenye mikopo inayoweza kuitoa tu;
- (b) kuwa na sera ambayo imeweka viwango vya udhamini wa mikopo kabla ya kuingia kwenye makubaliano ya kushirikiana katika mikopo;
- (c) kushiriki tu katika mikopo inayotolewa kwa wanachama wa SACCOS inayokopa;
- (d) kushikilia nakala halisi ya mkataba wa kushirikiana katika mikopo au nakala yake pamoja na jedwali la urejeshaji mkopo; na
- (e) kupata idhini ya wajumbe wa Bodi kwa ajili ya kuruhusu kuendelea kutoa mkopo kwa mkopeshaji halisi.

Mikopo  
chechefu

39.-(1) SACCOS itachukulia kuwa mkopo ni chechefu endapo-

- (a) malipo yaliyofanyika ni kidogo kuliko rejesho kamili lililipaswa kulipwa;
- (b) mkupuo mmoja wa rejesho haujalipwa kuendana na masharti ya mkataba;
- (c) mkopaji hajalipa rejesho kwa zaidi ya siku thelathini pale ambapo rejesho hilo ni riba au mkopo halisi; au
- (d) ikiwa ni mkopo unaolipwa kwa mkupuo mmoja, jumla ya deni la msingi na riba havijalipwa ndani ya siku thelathini mara baada ya kupita kwa muda wa marejesho.

(2) Salio lote la msingi la mkopo unaolipwa kwa mkupuo mmoja litachukuliwa kuwa ni chechefu endapo rejesho ambalo halijalipwa lilikua ni riba peke yake.

(3) Endapo mjumbe wa SACCOS ameshindwa kulipa mkopo wote au awamu moja ya marejesho mjumbe huyo hatapewa tena mkopo mpaka alipe deni lililopo.

Uanishaji wa makundi na tengo la mikopo

40.-(1) Kila SACCOS itagawa orodha ya mikopo yake kwenye makundi yafuatayo-

- (a) iliyo ndani ya muda;
- (b) angalizo;
- (c) chini ya kiwango;
- (d) mashaka na;
- (e) hasara.

(2) Vigezo vya makundi ya orodha ya mkopo itakuwa kama ifuatavyo-

Idadi ya siku zilizocheleweshwa	Kundi
Siku 0 mpaka 30	Iliyo ndani ya muda
Siku 31 mpaka 90	Angalizo
Siku 91 mpaka 180	Chini ya kiwango
Siku 181 mpaka 365	Mashaka
Zaidi ya siku 365	Hasara

(3) Kiwango cha chini cha tengo kwa kila kundi kitakuwa kama ifuatavyo-

Makundi	Tengo
Angalizo	10%
Chini ya kiwango	30%
Mashaka	50%
Hasara	100%

Limbikizo la riba ya mikopo chechefu

41.-(1) SACCOS itasitisha limbikizo la riba ya mikopo chechefu na tangulizi endapo mikopo hiyo imecheleweshwa kwa siku tisini.

(2) Limbikizo lolote la riba ambalo halijakusanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) litaondolewa na kuwekwa kwenye akaunti ya muda.

(3) SACCOS inaweza kurudisha mkopo kutoka katika hali isiyolimbikizwa na kwenda kwenye hali ya kulimbikizwa

endapo mkopaji amelipa amefuata masharti.

Kurekebisha  
masharti ya  
mikopo

42.-(1) Kwa mujibu sera yake ya mikopo, SACCOS inaweza kurekebisha masharti ya mkopo kwa kuzingatia kuwa-

- (a) mkopo hautarekebishwa zaidi ya mara moja; na
- (b) mkopo hautapandishwa hadhi isipokuwa pale ambapo mkopaji amelipa mikupuo minne mtawalia na kwa wakati.

(2) SACCOS itatoa taarifa ya mikopo yote iliyorekebishwa katika mstari wa peke yake katika taarifa ya hali ya kifedha.

Ufutaji wa  
mikopo

43.-(1) Kwa mujibu wa sera yake ya mikopo, SACCOS itafuta mikopo pale ambapo-

- (a) mkopo ni chechefu kwa zaidi ya mwaka mmoja;
- (b) SACCOS imepoteza haki zake za kimkataba juu ya mkopo husika;
- (c) imebainika kuwa mkopo hauwezi kulipika;
- (d) hakuna matarajio ya marejesho ya mkopo kufuatia maamuzi ya mahakama dhidi ya mkataba wa ukopeshaji;
- (e) dhamana zinazoshikiliwa zimefanyiwa tathmini na kuuzwa lakini mauzo yaliyopatikana hayatoshi kulipa deni lote;
- (f) SACCOS haina uwezo wa kukusanya mkopo na hakuna dhamana.

(2) Endapo mkopo umefutwa chini ya Kanuni hizi, SACCOS itahakikisha kuwa-

- (a) taarifa za mkopo huo zinahifadhiwa nje ya mizania;
- (b) jitihada za ukusanyaji wa mkopo huo zinaendelea; na
- (c) taarifa za mkopo huo zinatunzwa kwa usiri.

SEHEMU YA SITA  
USIMAMIZI WA UKWASI, MALI NA DHIMA

Sera ya  
usimamizi wa  
mali na dhima

44.-(1) Kila SACCOS itatunga sera ya usimamizi wa ukwasi, mali na dhima.

(2) Sera inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa uchache itajumuisha yafuatayo-

- (a) mtu atakayehusika kusimamia ukwasi, mali na dhima;
- (b) njia na kiasi kitakachotumika kusimamia ukwasi ikijumuisha uwiano uliowekwa katika Kanuni hizi;
- (c) kiwango cha juu cha fedha taslimu kinachopaswa kuwepo;
- (d) utaratibu wa mara kwa mara wa kuchambua hali ya ukwasi, mali na dhima; na
- (e) mpango wa dharura wa ukwasi.

(3) Sera inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1), itafanyiwa mapitio kila mwaka kuhakikisha kwamba inabaki kuwa halisia na yenye kufuata utaratibu.

(4) Sera ya usimamizi wa ukwasi, mali na dhima itawasilishwa Benki au Mamlaka Kasimishwa siyo zaidi ya siku thelathini baada ya kuwa imeidhinishwa na Bodi, na pale ambapo kuna mabadiliko yoyote yamefanywa katika sera, SACCOS itaonyesha bayana maeneo yote yaliyoguswa na mabadiliko hayo.

Mpango wa dharura wa ukwasi

45.-(1) SACCOS itaandaa na kuwasilisha Benki au Mamlaka Kasimishwa nakala ya mpango wa dharura wa ukwasi ulioidhinishwa na bodi kwa ajili ya kukabiliana na hali ya upungufu wa fedha.

(2) Mpango wa dharura wa ukwasi, kwa uchache utajumuisha taratibu za kurekebisha mapungufu ya fedha katika mzunguko, vyanzo vya fedha vinavyotegemewa, tathimini ya gharama za mikakati mbadala ya kupata fedha na athari zake katika mtaji wa SACCOS.

Kiwango cha chini cha uwiano wa ukwasi wa mali

46.-(1) SACCOS itatakiwa kuwa na kiwango cha chini cha ukwasi wa mali kisichopungua asilimia kumi na tano ya akiba, amana, mikopo ya muda mfupi na madeni ya muda mfupi ya wanachama wake.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, “ukwasi wa mali” unajumuisha-

- (a) noti na sarafu ambazo ni pesa halali katika Jamhuri ya Muungano;

- (b) amana zilizo katika benki au kwa watoa huduma ndogo za fedha;
- (c) dhamana za serikali za muda mfupi na muda mrefu ambazo zinaweza kuuzwa kwenye soko na kurudishwa kuuzwa Benki, na
- (d) mali nyingine zozote ambazo Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuainisha.

Amana katika benki

47. Isipokuwa kama imeruhusiwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa, SACCOS haitaweka amana zinazozidi asilimia ishirini na tano ya mtaji tete kwenye benki moja au taasisi za fedha.

Ukopaji nje ya SACCOS

48.-(1) Baada ya kupata idhini ya mkutano mkuu, SACCOS inaweza kukopa kutoka vyanzo vya nje, kwa kuzingatia kuwa-

- (a) mkopo huo umeidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa; na
- (b) jumla ya mikopo yake ya nje haizidi asilimia ishirini na tano ya jumla ya mali.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, “ukopaji wa nje” maana yake ni ukopaji kutoka nje ya wanachama ikijumuisha benki na taasisi za fedha.

Sera ya uwekezaji

49.-(1) Kila SACCOS itatunga sera ya uwekezaji.

(2) Sera iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itajumuisha angalau yafuatayo-

- (a) uwekezaji unaoruhusiwa kwa mujibu wa sheria husika;
- (b) ukomo wa uwekezaji kwa kila eneo la uwekezaji;
- (c) utambuzi wa vihatarishi na mikakati ya kuvipunguza;
- (d) watu walio na mamlaka ya kufanya uwekezaji;
- (e) aina na vipindi vya uwasilishaji wa taarifa bodi; na
- (f) taratibu za uidhinishaji na ukomo wake.

(3) Sera inayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa ajili ya kuidhinishwa na itafanyiwa mapitio kila mwaka kuhakikisha

kwamba sera inabaki kuwa halisia na yenye kufuata utaratibu.

Masharti ya uwekezaji

50.-(1) SACCOS haitafanya uwekezaji isipokuwa kama uwekezaji huo-

Sura ya 211

- (a) unazingatia sera ya uwekezaji iliyoidhinishwa;
- (b) unazingatia masharti ya Sheria ya Vyama vya Ushirika;
- (c) umeidhinishwa na mkutano mkuu wa SACCOS;
- (d) ikiwa ni uwekezaji wa kifedha, uliofanywa kwa lengo la kuwekwa hadi kufikia kipindi cha kuiva.

(2) SACCOS inaweza kuwekeza katika-

- (a) amana zilizo na riba kwenye benki au taasisi za fedha;
- (b) dhamana za Serikali;
- (c) SACCOS nyingine;
- (d) mali zisizozalisha; au
- (e) uwekezaji mwingine wowote kama itakavyoidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Endapo SACCOS itawekeza katika mali zisizozalisha, uwekezaji huo hautazidi-

- (a) asilimia kumi ya jumla ya mali zake iwapo uwekezaji umefanyika kwenye mashine au vifaa; na
- (b) asilimia tano ya jumla ya mali zake iwapo uwekezaji umefanyika kwenye ardhi na majengo, isipokuwa pale ambapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imetoa ruhusa maalumu.

#### SEHEMU YA SABA HESABU NA UKAGUZI

Vitabu vya hesabu, kumbukumbu na mwaka wa fedha

51.-(1) SACCOS itatunza vitabu vya hesabu vilivyo sahihi pamoja na kumbukumbu nyingine kuhusu shughuli zake ambazo zinatoshleza kuonyesha na kueleza miamala na hali yake ya kifedha.

(2) Vitabu vya hesabu na kumbukumbu



vinavyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1)-

- (a) vitaelezea kwa ufasaha miamala yote ikiwemo maombi na miamala yote ya mikopo;
- (b) zitaiwezesha hali ya kifedha ya SACCOS kujulikana kwa usahihi wakati wowote;
- (c) zitawezesha uandaaji wa taarifa za fedha kwa wakati;
- (d) zitajumuisha nyaraka za msingi ambazo zinahifadhiwa ili kuakisi taarifa za-
  - (i) jumla ya fedha zote zilizopokelewa na kutumika na masuala yanayohusu mapato na matumizi yaliyofanyika;
  - (ii) mauzo, manunuzi yote na miamala mingine; na
  - (iii) mali na madeni ya SACCOS.

(3) Kwa madhumuni ya uhasibu, ukaguzi na utoaji wa taarifa, mwaka wa fedha wa SACCOS utanza tarehe 1 Januari na kuisha 31 Disemba ya kila mwaka.

Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu

52. Kila SACCOS, katika kila mwaka wa fedha, itaandaa hesabu na ndani ya miezi minne kuanzia mwisho wa mwaka wa fedha kuwasilisha Benki au Mamlaka Kasimishwa, nakala za hesabu za mwaka zilizokaguliwa na taarifa ya ukaguzi.

Uwekaji wa taarifa za fedha

53.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria, kila SACCOS itaweka wazi katika sehemu yake ya biashara nakala ya taarifa zake za fedha zilizokaguliwa hivi karibuni.

(2) Taarifa za fedha zilizokaguliwa zinazotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1)-

- (a) zitajumuisha mizania, taarifa za mapato, taarifa za mtiririko wa fedha na taarifa za mabadiliko ya mtaji;
- (b) zitawekwa eneo la wazi katika sehemu kuu ya biashara, matawi na vituo vya nje vya huduma; na
- (c) zitawekwa wazi kwa kipindi chote cha mwaka.

Uteuzi wa mkaguzi wa ndani

54.-(1) SACCOS itamteua mkaguzi wa ndani katika kutathmini utoshelevu na ufanisi wa uhibititi wa ndani,

udhibiti wa vihatarishi na mifumo ya utawala.

(2) Mkaguzi wa ndani anayeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atakuwa na, angalau, stahahada ya uhasibu au sifa inayofanana na hiyo na awe na uzoefu wa angalau mwaka mmoja katika fani husika.

Utoaji taarifa  
wa mkaguzi  
wa ndani

55.-(1) Mkaguzi wa ndani atawajibika kwa Bodi.  
(2) Taarifa za mkaguzi wa ndani zitakuwa na hoja za ukaguzi, mapendekezo na mrejesho kutoka menejimenti.

Majukumu ya  
mkaguzi wa  
ndani

56. Majukumu ya mkaguzi wa ndani yatajumuisha-

- (a) kuhakiki fedha bila kutoa taarifa ya awali pale inapolazimu;
- (b) kufanya upatanisho wa akaunti ya benki;
- (c) kufanya upatanisho wa kati ya salio la leja kuu na salio la leja ndogo;
- (d) kukagua majalada ya mikopo kwa ajili ya kuangalia uzingatiwaji wa taratibu;
- (e) uhakiki wa mali na uwekezaji wa SACCOS;
- (f) kukagua utoshelevu wa masharti ya mikopo isiyolipika;
- (g) kukagua uzingatiaji wa sera na taratibu;
- (h) kukagua uzingatiaji wa Sheria na sheria nyingine husika;
- (i) kutathmini usahihi na ukamilifu wa mihtasari na taarifa za menejimenti kwenda kwa Bodi na kamati;
- (j) kutathmini utoshelevu wa mfumo wa usimamizi wa taarifa;
- (k) kutathmini usahihi na uaminikajiwa taarifa za ukaguzi na taarifa za fedha;
- (l) kubaini iwapo taarifa na maelezo yanayowasilishwa Benki au Mamlaka Kasimishwa ni sahihi na hutolewa kwa wakati;
- (m) kubaini iwapo taratibu za uhasibu na mifumo ya udhibiti inatosheleza;
- (n) kuhakiki utekelezaji na uwekaji wa mifumo thabiti ya ndani inayofaa kwa menejimenti;
- (o) kuhakikisha kuwa hoja na mapendekezo yote ya

wakaguzi wa hesabu wa ndani na nje na yanatekelezwa; na  
(p) kutathmini ufanisi wa matumizi ya rasilimali.

Mpango wa ukaguzi wa ndani

57.-(1) Mkaguzi wa ndani ataandaa mpango wa ukaguzi wa mwaka kwa ajili ya kazi zitakazofanywa katika mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Mpango wa ukaguzi unaotajwa katika kanuni ndogo ya (1) utajumuisha angalau-

- (a) muda na vipindi vilivyopangwa kwa kazi ya ukaguzi wa ndani;
- (b) tathmini ya udhibiti wa ndani;
- (c) maelezo muhimu ya rasilimali watu na rasilimali nyingine; na
- (d) muda uliotengwa kwa ajili ya mafunzo.

(3) Mpango wa ukaguzi wa mwaka utawasilishwa kwa kamati ya usimamizi kwa ajili ya mapitio na kwa Bodi kwa ajili ya kupata idhini kabla ya tarehe 31 Disemba kila mwaka.

Kukodi mkaguzi wa ndani

58. SACCOS inaweza kukodi huduma ya ukaguzi wa ndani kutoka kwa kampuni ya ukaguzi iliyosajiliwa au mtu binafsi mwenye sifa ikizingatiwa kwamba, kampuni ya ukaguzi au mtu binafsi mwenye sifa atafanya kazi za ukaguzi wa ndani kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Ukaguzi wa nje

59.-(1) Hesabu za SACCOS zitakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na COASCO au mkaguzi mwingine wa nje mwenye uwezo na aliyesajiliwa ambaye ameteuliwa na mkutano mkuu na kuidhinishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(2) Endapo SACCOS itashindwa kuteua mkaguzi wa nje wa hesabu au kujaza nafasi yeyote kwa ajili ya mkaguzi wa nje ambayo inaweza kujitokeza, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuteua, kwa niaba ya SACCOS, mkaguzi wa nje na kupanga malipo yake ambayo yatalipwa na SACCOS.

(3) SACCOS haitakuwa bila mkaguzi wa nje kwa zaidi ya siku tisini kuanzia tarehe nafasi hiyo ilipokuwa wazi.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), mkaguzi wa nje hatafanya ukaguzi wa nje wa SACCOS kama mkaguzi huyo-

(a) ana uhusiano na maafisa au waajiriwa wa SACCOS; au

(b) ni mwanachama wa SACCOS husika.

Mkaguzi wa nje kuwafikia waajiriwa

60. Wakaguzi wa nje wanaweza kufanya mazungumzo na afisa wa SACCOS au afisa aliyekuwa ameajiriwa na SACCOS au mwajiriwa wa SACCOS kwa lengo la kupata taarifa muhimu kwa ajili ya ukaguzi husika.

Kutoa taarifa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa

61. Mkaguzi wa nje atatoa taarifa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa juu ya mapungufu yoyote au matendo yanayokiuka Sheria yaliyotendwa na maafisa wa SACCOS, waajiriwa au kwa namna nyingine itakavyokuwa.

Kuwasilisha taarifa ya ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka

62. Mkaguzi wa nje atawasilisha taarifa za fedha zilizokaguliwa na taarifa ya ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Kubadilisha mkaguzi wa nje

63. SACCOS haitaruhusiwa, wakati zoezi la ukaguzi linaendelea, kumbadilisha mkaguzi wa nje isipokuwa pale itakapopata idhini ya maandishi kutoka Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Kipindi cha mkaguzi wa nje

64.-(1) Mkaguzi wa nje mbali na COASCO hatakagua SACCOS moja kwa zaidi ya kipindi cha miaka mitatu mtawalia.

(2) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), mkaguzi wa nje, mbali na COASCO, anaweza kuendelea na kazi ya ukaguzi wa nje kwa SACCOS ileile baada ya kupita miaka miwili tokea alipofanya ukaguzi wa mwisho.

SEHEMU YA NANE  
UKAGUZI NA USIMAMIZI

Ukaguzi wa  
SACCOS

65.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa katika kutumia mamlaka yake ya ukaguzi chini ya kifungu cha 13 cha Sheria, itafanya ukaguzi wa SACCOS.

(2) Ukaguzi unaorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) utajumuisha yafuatayo-

(a) kuhakikisha SACCOS inatekeleza masharti na sera zake katika uendeshaji wa shughuli zake;

(b) kukagua uendeshaji na hali ya kifedha ya SACCOS;

(c) kutathimini ufanisi wa udhibiti uliopo dhidi ya uendeshaji, fedha na mali nyingine za SACCOS;

(d) kuchambua taarifa za mara kwa mara zinazowasilishwa na SACCOS ; na

(e) masuala mengine yoyote kama yanavyoweza kuainishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Baada ya kukamilisha ukaguzi chini ya kanuni ndogo ya (1), Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuandaa na kuwasilisha nakala ya taarifa ya ukaguzi kwa Bodi au mkutano mkuu wa SACCOS.

(4) Bodi ya SACCOS itahakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa kushughulikia masuala yaliyoibuliwa katika taarifa ya ukaguzi.

(5) Taarifa ya ukaguzi iliyoandaliwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa itakuwa ni ya siri.

Uchunguzi

66.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza, baada ya kuombwa au kupitia maombi ya mwanachama au mdai wa SACCOS au baada ya kupokea taarifa hasi kutoka chanzo chochote, kufanya uchunguzi wa masuala ya uendeshaji au kifedha wa SACCOS.

(2) Baada ya kukamilisha uchunguzi uliofanywa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuandaa na kuwasilisha nakala ya taarifa ya uchunguzi kwa Bodi au mkutano mkuu wa SACCOS na taarifa hiyo itakuwa ni ya siri.

(3) Endapo baada ya uchunguzi, Benki au Mamlaka Kasimishwa itabaini kasoro, mapungufu, hasara au makosa yaliyofanywa na wajumbe wa Bodi au menejimenti, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuchukua hatua stahiki za kiutawala kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Uwasilishaji  
wa taarifa

67. SACCOS itawasilisha kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa taarifa za mara kwa mara kwa mfumo na vipindi vitakavyoanishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Makubaliano  
ya pamoja ya  
usimamizi

68.-(1) Endapo itabainika kwamba SACCOS haifanyi vizuri na taratibu za usimamizi za kawaida zimeshindwa kurekebisha hali iliyopo, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuingia katika makubaliano ya pamoja ya usimamizi na Bodi ya SACCOS ili kurekebisha mapungufu hayo.

(2) Makubaliano ya pamoja yaliyofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) yataweka hatua mahsusi za marekebisho au maboresho ndani ya muda ulioainishwa na yatasainiwa na Bodi na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Endapo SACCOS itashindwa kutekeleza hatua zilizoainishwa ndani ya muda wa makubaliano ya pamoja, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kufuta leseni yake.

Utoaji wa  
amri ya zuio  
na katazo

69.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kutoa amri ya zuio na katazo kuielekeza SACCOS kushughulikia mienendo iliyo hatarishi au isiyofaa ambayo haijashughulikiwa ipasavyo kupitia hatua nyingine za usimamizi.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kutoa amri ya zuio na katazo pale ambapo SACCOS-

- (a) imejihusisha au inaendelea kujihusisha na mienendo yoyote ya kibiashara iliyo hatarishi;
- (b) imekiuka au inaendelea kukiuka Sheria, Kanuni hizi, masharti au sera zake; au
- (c) imeshindwa au inaendelea kushindwa kuzingatia Makubaliano ya Pamoja ya Usimamizi.

Usimamizi na  
kutwaa  
uendeshaji

70.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kutwaa usimamizi wa SACCOS pale ambapo-

- (a) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaona kuwa SACCOS husika-
  - (i) haipo katika hali nzuri kifedha;
  - (ii) haijiendeshi kwa mujibu wa misingi na taratibu stahiki za utawala na uhasibu;
  - (iii) haizingatii sera sahihi za udhibiti wa vihatarishi; au
  - (iv) haizingatii maelekezo yanayotolewa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.
- (b) SACCOS imeshindwa kuzingatia masharti ya kiwango cha chini cha mtaji kilichoainishwa katika Kanuni hizi;
- (c) SACCOS imekataa kukaguliwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa kama inavyotakiwa na Sheria;
- (d) leseni ya SACCOS imefutwa; au
- (e) SACCOS inaendesha biashara ya huduma ndogo za fedha kwa namna ambayo ni kinyume na Sheria au inaathiri maslahi ya wanachama.

(2) Baada ya kutwaa uendeshaji chini ya kanuni ndogo ya (1), Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kutumia huduma ya watu binafsi kusimamia SACCOS iwapo Benki au Mamlaka Kasimishwa itaona kwamba kufanya hivyo ndio njia sahihi, fanisi na ya gharama nafuu.

(3) Gharama za usimamizi wa SACCOS katika kipindi cha kutwaa usimamizi zitalipwa na SACCOS husika.

(4) Katika kipindi cha usimamizi hakuna mali yoyote ya SACCOS itakayoshikiliwa au kuhusishwa na dai la umiliki isipokuwa dai la umiliki lililowekwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Ukomo wa  
usimamizi wa  
Benki au  
Mamlaka  
Kasimishwa

71.-(1) Usimamizi wa Benki au Mamlaka Kasimishwa utakoma pale ambapo hali ya kifedha na kiuendeshaji ya SACCOS imeimarika au ndani ya miezi sita, chochote kitakachotangulia.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuongeza kipindi cha miezi sita kinachotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) endapo hali ya kifedha na uendeshaji wa SACCOS hajaimarika.

(3) Mabadiliko yote yatakayofanywa na Benki au Mamlaka Kasimishwa katika sera, taratibu au usimamizi wa SACCOS katika kipindi cha usimamizi yatabaki kuwa halali hata baada ya kukoma kwa usimamizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(4) Benki au Mamlaka Kasimishwa itatoa amri ya ufilisi kwa mujibu wa sheria endapo hali ya kifedha na shughuli za SACCOS hazijaimarika baada ya kuisha kwa miezi sita au muda wa nyongeza uliotolewa na Benki au Mamlaka Kasimishwa chini ya kanuni ndogo ya (2).

#### SEHEMU YA TISA KUMLINDA MLAJI

Masharti ya  
uwazi wa  
hisa, akiba na  
amana

72.-(1) Kila SACCOS itapaswa kuweka bayana kwa maandishi vigezo na masharti kuhusiana na kila hisa, akiba na amana za muda maalum kwa wanachama wake na wanachama tarajiwa.

(2) SACCOS itatoa taarifa za akaunti za hisa, akiba au amana kwa mwanachama anayeomba.

(3) Endapo akaunti itakuwa inamilikiwa na mwanachama zaidi ya mmoja au mkopo umetolewa kwa mwanachama zaidi ya mmoja, taarifa inaweza kutolewa kwa yeyote kati yao.

(4) Kwa akaunti zinazostahili gawio, SACCOS inaweza kuweka bayana viwango vya gawio vilivyopita au vinavyotarajiwa na asilimia ya mapato tarajiwa ya mwaka na njia iliyotumika kukokotoa gawio.

Uwazi kwa  
akaunti zenye  
riba

73.-(1) SACCOS itaweka wazi kiwango cha riba kilichopo na asilimia ya mapato ya mwaka kama ilivyoelezwa na bodi na njia iliyotumika kukokotoa riba.

(2) Taarifa yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itaeleza bayana iwapo akaunti ina viwango vya riba vinavyobadilika au visivyobadilika.

(3) Taarifa yoyote iliyotolewa kuhusiana na akaunti ya kiwango cha riba kisichobadilika itaonyesha muda ambao kiwango hakitabadilika na muda ambapo kiwango kitaanza kulimbikizwa na malipo ya riba kufanyika.



(4) Kwa akaunti zenye viwango vinavyobadilika, uwazi huo utaeleza yafuatayo-

- (a) kwamba kiwango cha riba kinaweza kubadilika;
- (b) jinsi kiwango cha riba kinavyokokotolewa;
- (c) iwapo kuna kielelezo kilichotumika kuandaa kiwango kinachobadilika; na
- (d) muda ambapo riba itanza kulimbikizwa na kipindi kiwango kitabadilika.

Uwazi wa taarifa za ziada

74. Pamoja na mahitaji ya taarifa za ziada chini ya Kanuni ya 72, SACCOS itatoa taarifa zifuatazo-

- (a) vipindi vya gawio au ukokotoaji wa riba na wakati ambapo gawio au riba italipwa;
- (b) zuio la gawio au riba kwa wanachama pale wanapofunga akaunti zao kabla malipo ya gawio au riba kuingizwa kwenye akaunti;
- (c) masharti ya salio la chini la kufungua akaunti;
- (d) ada zinazoambatana na kila aina ya akaunti na mazingira ambayo ada inaweza kutozwa;
- (e) zuio lolote la kutoa fedha; na
- (f) huduma au bidhaa zote zitolewazo kwa wanachama wake.

Uwazi wa mabadiliko ya masharti ya akaunti

75. SACCOS itatoa notisi ya awali ya maandishi kwa wanachama walioathirika na mabadiliko yaliyofanywa katika akaunti endapo-

- (a) mabadiliko yanapunguza asilimia ya mapato kwa mwaka kwa akaunti za hisa na akiba; au
- (b) masharti ya hisa au akiba yamebadilika.

Uwazi katika utoaji wa mkopo

76. SACCOS itahakikisha kuna uwazi na utoaji wa kutosha wa taarifa za bidhaa na huduma kwa kuhakikisha kwamba, mkataba wa mkopo-

- (a) unasomeka na umeandikwa kwa lugha rahisi na inayoeleweka; na
- (b) una vigezo na masharti ambayo ni ya wazi, ya usawa na yanayolinda haki za mkopaji.

Mfumo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro

77.-(1) Kila SACCOS itakuwa na mfumo wa kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro ambao kwa uchache utajumuisha-

- (a) namna ya kuwasilisha malalamiko;
- (b) uanzishwaji wa dawati au kuteua afisa ambaye atashughulikia malalamiko;
- (c) kipindi cha kushughulikia migogoro na kutoa mrejesho.

(2) Kila SACCOS itahakikisha kwamba mfumo wa kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro kwa wateja na taarifa za mawasiliano husika zinajumuisha namba za simu au barua pepe zinaonyeshwa kwa dhahiri katika sehemu kuu ya biashara, matawi na vituo vya huduma vilivyo wazi kwa umma.

(3) Taarifa zinazotajwa chini ya kanuni ndogo ya (2), zitakuwa katika lugha ya Kiswahili au lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza.

Uwazi kwa wadhamini wa mikopo

78. SACCOS itampa mdhamini taarifa ya maandishi, ikionyesha wajibu wake juu ya mkopo alioudhamini na taarifa hiyo itajumuisha-

- (a) jina na anwani ya SACCOS;
- (b) namba ya mkopo;
- (c) jina la mkopaji;
- (d) kiasi cha mkopo;
- (e) tarehe mkopo ulipotolewa; na
- (f) saina ya mdhamini.

Kukusanya au kufuatilia mikopo

79.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria, SACCOS itakusanya au kufuatilia mkopo kutoka kwa mkopaji kwa mujibu wa taratibu za makusanyo kama zilivyoainishwa kwenye sera ya mikopo.

(2) Kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba taratibu za kukusanya au kufuatilia mkopo zinazingatia misingi ya kumlinda mlaji, SACCOS-

- (a) itatoa notisi ya maandishi ya siku kumi na nne kwa mkopaji kabla ya utaratibu wa kukusanya au kufuatilia deni haujaanza;
- (b) haitamnyanya, kumtukana au kumkandamiza mkopaji, mdhamini au mtu yeyote anayehusika na ukusanyaji au ufuatiliaji wa deni;
- (c) haitomtisha au kutumia nguvu au njia haramu katika kukusanya au kufuatilia deni;

- (d) haitotumia lugha ya matusi au lugha isiyofaa;
- (e) haitotumia maelezo au njia za uongo, udanganyifu au kupotosha au njia kama-
  - (i) kutoa taarifa ya uongo ya tabia ya mhusika, kiwango, kiasi, au hadhi ya kisheria ya deni lolote;
  - (ii) kutoa maelezo ya uongo kwamba mhusika ni wakili au mawasiliano yoyote yaliyofanywa yametoka kwa wakili;
  - (iii) kutishia kuchukua hatua yoyote ambayo haiwezi kuchukuliwa kisheria au kukusudiwa kuchukuliwa; au
  - (iv) kuwasiliana au kutishia kufanya mawasiliano kwa mtu yeyote kuhusu taarifa za mkopo ambazo zinajulikana kuwa ni za uongo.
- (3) SACCOS haitakusanya riba, ada, tozo, au gharama isipokuwa kama zimeainishwa katika mkataba wa mkopo.
- (4) SACCOS inaweza kumtumia mkusanya madeni kukusanya au kufuatilia mkopo kutoka kwa mwanachama endapo mkusanya madeni huyo-
  - (a) amesajiliwa na Tume;
  - (b) anakusanya au kufuatilia madeni kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (2) na ya (3) ya kanuni hii; na
  - (c) anazingatia sheria husika zinazosimamia ukusanyaji madeni.

Elimu ya fedha

- 80.-(1) SACCOS itatoa elimu ya fedha kwa wanachama wake ambayo kwa uchache itajumuisha mambo yafuatayo-
- (a) sifa muhimu za bidhaa na huduma zinazotolewa;
  - (b) vigezo na masharti ya mikopo;
  - (c) usimamizi wa mtiririko wa fedha;
  - (d) utunzaji wa kumbukumbu;
  - (e) maamuzi ya masuala ya fedha;
  - (f) usimamizi mikopo, matumiazi na marejesho;
  - (g) mpango wa biashara;
  - (h) umuhimu wa kuweka akiba; na
  - (i) masuala mengine yoyote yanayoonekana ni

muhimu.

- (2) Elimu ya fedha inayotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaweza kutolewa kupitia-
- (a) vikao vya mtu mmoja mmoja;
  - (b) vipeperushi na vijarida;
  - (c) mafunzo;
  - (d) semina;
  - (e) kongamano;
  - (f) vyombo vya habari kama vile runinga, redio na magazeti;
  - (g) mitandao ya kijamii au tovuti maalum;
  - (h) vikao vya ushauri nasaha; na
  - (i) njia nyingine yoyote kama itakavyoonekana inafaa.

Uzingatiji wa sheria za kumlinda mlaji

81. Bila kujali sharti lolote katika Kanuni hizi, SACCOS itazingatia sheria zinazohusu kumlinda mlaji katika masuala ya fedha.

**SEHEMU YA KUMI  
MASHARTI YA JUMLA**

Mpango wa uendelezaji biashara

82.-(1) SACCOS itaandaa mpango wa uendelezaji biashara.

(2) Mpango wa uendelezaji biashara utajumuisha kwa uchache yafuatayo-

- (a) mtu au watu wenye wajibu wa kutekeleza, kufuatilia, kuthaminisha na kufanya mapitio ya mpango;
- (b) wajibu na majukumu ya maafisa kufanya tathmini, kutoa taarifa na huduma kwa wanachama;
- (c) utambuzi wa maeneo mbadala yenye vitendea kazi muhimu kwa ajili ya kusaidia shughuli muhimu kuendelea kufanywa kwa muda wa kutosha iwapo kutatokea majanga;
- (d) utambuzi wa taarifa muhimu zinazohitajika kuendesha SACCOS kipindi cha majanga;
- (e) mpango wa usalama ulioandaliwa kwa ajili ya kulinda majengo ya SACCOS; na

(f) mpango mbadala wa nishati ya umeme.

(3) Mpango wa uendelezaji biashara utapitiwa na kujaribiwa angalau mara moja kwa mwaka.

Uwasilishaji  
wa taarifa za  
mikopo

83.-(1) Baada ya SACCOS kupata utambulisho sahihi wa wakopaji itatoa taarifa kamili kwa taasisi za ubadilishanaji taarifa za mikopo kuhusu mikopo yote iliyotolewa kwa kila mkopaji kwa namna ambayo Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuainisha.

(2) SACCOS itawasilisha kila mwezi taarifa za mikopo yote iliyopo na mipya iliyotolewa kwa mwanachama kwa taasisi za ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.

Tangazo la  
Serikali Na.  
416 la mwaka  
2012

(3) SACCOS itapata na kutumia taarifa za mikopo kupitia taasisi za ubadilishanaji taarifa za mikopo kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Taasisi za Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo).

(4) SACCOS itatoa taarifa za mikopo zilizokamilika, sahihi na kwa muda mwafaka.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, SACCOS itazingatia masharti ya Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Taasisi za Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo).

(6) Kwa madhumuni ya kanuni hii “taarifa za mikopo” maana yake ni taarifa zozote zikijumuisha taarifa zinazohusu utambulisho wa mtu, jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, eneo la makazi, maeneo ya makazi ya awali, hali ya ndoa, jina la mwenza, sehemu ya kazi, sehemu za kazi za awali, mwenendo wa ulipaji, madeni yaliyopo, mali na maulizo ya historia za mikopo au taarifa zinazohusu taasisi au biashara ambazo zitasaidia kutambua taasisi au taarifa za biashara zinazohusu usajili, kodi, wakurugenzi, utawala, madeni yaliyopo, mali, maulizo ya historia ya madeni na taarifa nyingine za biashara.

Ridhaa ya  
kubadilishana  
taarifa za  
mikopo

84. SACCOS itahakikisha kwamba wakopaji wote wameridhia kwa maandishi kuiruhusu SACCOS kupata, kubadilishana au kuweka wazi taarifa zote za mikopo zinazohusu wakopaji, wakopeshaji au taasisi za ubadilishanaji taarifa za mikopo.

Hatua za  
kiutawala

85.-(1) Bila kuathiri adhabu na hatua zilizoainishwa chini ya Sheria, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuchukua hatua zifuatazo za kiutawala dhidi ya SACCOS iliyokiuka masharti-

- (a) kuweka zuio la kutangaza au kulipa gawio;
- (b) kuweka zuio la kufungua au kuanzisha matawi au vituo vya nje vya huduma;
- (c) kusitisha shughuli za ukopesaji na uwekezaji;
- (d) kufuta leseni;
- (e) onyo rasmi kwa mjumbe wa Bodi au meneja aliyekiuka taratibu;
- (f) kumsimamisha mjumbe wa Bodi au mtendaji mwandamizi aliyekiuka masharti;
- (g) kumwondolea sifa ya kuendelea kushikilia cheo au nafasi yoyote katika SACCOS yeyote iliyo chini ya usimamizi wa Benki au Mamlaka Kasimishwa;
- (h) adhabu ya kulipa kiasi cha fedha kitakachoamuliwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa kisichopungua shilingi laki tano na kisichozidi shilingi milioni tano; au
- (i) hatua nyingine zozote za kiutawala kama Benki au Mamlaka Kasimishwa itakavyoelekeza.

(2) Hatua zinazotajwa katika kanuni ndogo ya (1)(a) itatumika kwa wakurugenzi, maafisa au waajiriwa wa SACCOS.

Kuhama  
daraja kwa  
SACCOS

86.-(1) SACCOS inaweza, baada ya kufanya maombi na kufikia vigezo vilivyoanishwa katika Kanuni husika au sheria husika, kuhama kutoka Daraja la 3 kwenda Daraja la 2 au Daraja la 1.

(2) SACCOS haitatuma maombi ya kuhama daraja kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) isipokuwa-

- (a) SACCOS husika imetoa taarifa kwa maandishi kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa juu ya dhamira ya kuhama daraja; na
- (b) wanachama wake wamedhamiria kuhama daraja kwa kuzingatia katiba au masharti yake.

Kipindi cha mpito

87.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 57 cha Sheria, SACCOS ambayo ilikuwa ikifanya shughuli za huduma ndogo za fedha kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria na ambayo imeshindwa kukidhi masharti ya kupata leseni ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kuanza kutumika kwa Sheria, itafunga biashara yake na kukoma kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha.

(2) Mtu ambaye atakiuka kanuni hii atakua ametenda kosa na atakapopatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria.

Makubaliano kati ya SACCOS na waajiri

88.-(1) Endapo SACCOS inakusudia kutoa huduma kwa wanachama ambao ni waajiriwa wa taasisi yoyote na ambao hisa, akiba, amana na malipo yao ya mikopo ni kupitia makato ya mishahara ya waajiriwa, SACCOS husika-

(a) itaingia makubaliano na mwajiri yatakayoainisha yafuatayo-

(i) vigezo na masharti kwa ajili vya kukusanya hisa, akiba na amana;

(ii) masharti ya makato ya malipo ya mkopo kutoka mishahara ya waajiriwa na uwasilishaji wa makato kwa SACCOS;

(iii) majukumu ya mwajiri na SACCOS;

(iv) adhabu au suluhu za kisheria kwa ukiukwaji wa makubaliano; na

(v) masharti mengine yoyote husika;

(b) itahakikisha kwamba, makubaliano yaliyoingiwa yanawasilishwa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa ajili ya uhakiki.

(2) SACCOS ambayo itashindwa kuzingatia masharti ya kanuni hii itawajibika kwa hatua za kiutawala kama ambavyo Benki au Mamlaka Kasimishwa inaona inafaa.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii “huduma” inajumuisha ukusanyaji wa hisa, akiba, amana na utoaji wa mikopo.

*Kanuni Za Huduma Ndogo Za Fedha (Vyama Vvya Ushirika wa Akiba Na Mikopo)*

*Tangazo la Serikali Na. 966 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kanuni ya 5(1))*

FOMU YA MAOMBI YA LESENI

1. Jina la SACCOS: .....  
Na. ya Usajili ..... Tarehe ya Usajili .....
2. Mahali ilipo Ofisi Iliyosajiliwa .....
3. Anwani ya Ofisi ya Makao Makuu: Namba ya Usajili wa Ardhi (L.R.No.).....  
Mtaa .....  
Jengo.....
4. Sanduku la posta ..... Msimbo wa Posta .....  
Simu Na.....  
Barua pepe.....
5. Pale ambapo inafaa, majina ya maeneo ya biashara zilizopo Tanzania, mwaka zilipoanzishwa na miaka katika biashara.

<i>Na.</i>	<i>Jina la Tawi/Wakala/ Kituo cha Huduma</i>	<i>Mwaka ilipoanza</i>	<i>Idadi ya Miaka katika biashara</i>
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			

6. Pale ambapo inafaa, orodha ya maeneo mengine ya biashara. Weka jina la mahali pa biashara, taja endapo ni huduma zinazohamishika; mashine ya kutolea fedha (ATM) au sehemu ya mauzo nk.
7. Jina au majina ya awali, kama lipo/yapo, na ambalo/ambayo SACCOS ilijulikana kama
  1. .... kuanzia..... hadi .....
  2. .... kuanzia..... hadi .....
  3. .... kuanzia..... hadi .....



*Kanuni Za Huduma Ndogo Za Fedha (Vyama Vvya Ushirika wa Akiba Na Mikopo)*

*Tangazo la Serikali Na. 966 (Linaendelea.)*

4. .... kuanzia..... hadi .....

8. Maelezo ya Mtaji

(a) Thamani iliyolipwa .....

(b) Mtaji tete .....

(c) Mtaji taasisi .....

9. Taarifa za Maafisa:

a) Wajumbe wa Bodi

<i>Jina la Sasa na la Awali</i>	<i>Tarehe ya Kuzaliwa</i>	<i>Anwani</i>	<i>Tarehe ya Uteuzi</i>	<i>Ujumbe mwingine wa Bodi</i>
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				

(b) Watendaji Waandamizi

<i>Jina la Sasa na la Awali</i>	<i>Cheo</i>	<i>Tarehe ya kuzaliwa</i>	<i>Sifa za taaluma/ utaalum</i>	<i>Mwaka ulipopata</i>	<i>Tarehe ya uteuzi</i>	<i>Ajira/kazi ya awali</i>
1						
2						
3						
4						
5						
6						
7						

9. Majina ya Benki na anwani zake

1. .... S.L.P .....

2. .... S.L.P .....

3. .... S.L.P .....

4. .... S.L.P .....

*Kanuni Za Huduma Ndogo Za Fedha (Vyama Vvya Ushirika wa Akiba Na Mikopo)*

*Tangazo la Serikali Na. 966 (Linaendelea.)*

10. Je SACCOS imewahi kuwekwa chini ya ufilisi au kuingia muafaka wowote au utaratibu na wadai wake au kushindwa kuwalipa wadai kikamilifu? ..... Kama ndivyo, toa maelezo .....

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kanuni ya 8)*

LESENI NA. MSP3-

LESENI YA KUENDESHA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Imetolewa chini ya kifungu cha 21 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018

DARAJA.....

LESENI hii imetolewa kwa ..... (Jina la SACCOS)  
Na. ya Usajili .....ya ..... (Anwani)  
na inaidhinisha SACCOS husika kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha Tanzania Bara chini ya Daraja la 3 katika kundi.....la Leseni.

Leseni hii imetolewa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 na masharti yaliyoainishwa katika barua yetu yenye kumbukumbu Na. .... ya tarehe .....

Imetolewa leo..... tarehe .....

SAINI

Dar es Salaam,  
....., 2019

FLORENS LUOGA  
Gavana